



Kongamano la Kiswahili la 23

(Bayreuth, Tarehe 14 hadi 16 Mei, 2010)

22/01/10

Wapendwa Wahudhuria-Kongamano

Kwa mara nyingine tena, tuna furaha kubwa kukualikeni kushiriki katika Kongamano la Kiswahili litakalofanyika kuanzia tarehe 14 Mei, hadi 16 Mei, 2010.

Mwaka uliopita tulianzisha fikra ya *mada-kuu* katika uwasilishaji wa makala ya kongamano letu. Uitikiaji kutoka kwenu ulitushangaza na kutupa moyo kwa wingi na ubora wa makala yaliyowasilishwa. Mwaka huu, tunapenda kuiendeleza tena fikra hii ya *mada-kuu* kwa kupendekeza *Utamaduni Pendwa wa Kiswahili*.

Katika mwelekeo huu wa jumla, kama kawaida, tunategemea mchango wa *mada-teuzi* zitazoegeamea *Utamaduni Pendwa wa Kiswahili* na zitakazoainishwa kwa 'mitazamo ya taaluma kadha wakati mmoja', na 'mitazamo ya taaluma moja inavyoingiliana na taaluma nyingine'. Kwa hivyo, tungependa kupendekeza *mada-teuzi* zitokane na maeneo kadha kama vile: 'lahajajamii', 'lugha ya vijana mijini', 'riwaya ya upelelezi' au 'riwaya sisimuzi', 'ngonjera kama sanaa za maonyesho', 'sanaa za maonyesho kwa ajili ya maendeleo', 'filamu', 'miziki ya kimji', 'vikatuni', 'viponzo', 'vichapizo', 'mavazi', 'semi' n.k.

Ili tusiwaache nje wenzetu ambao, kwa sababu moja au nyingine, hawapendi kushughulikia *mada-kuu* ya *Utamaduni Pendwa wa Kiswahili*, tutakubali *mada-teuzi* yoyote itayohusu 'lugha ya Kiswahili', 'muundo wake', 'isimujamii', 'historia', 'ufundishaji' na vipengele vingine vya utamaduni wake'.

Hata hivyo, katika kongamano la mwaka huu, tutajipa uhuru wa kuamua mchango upi ukubalike na upi usikubalike. Kutokana na uamuzi huu tunakuombeni mutulettee anwani za *mada-teuzi* pamoja na vifupisho vyenu. Sisi tutapima viwasilisho hivyo kwa misingi wa ubora na tutawaarifu wote wale ambao viwasilisho vyao havitakubalika.

Katika mtazamo huu tunawakaribisha mjisajili kuanzia sasa hadi tarehe kuanzia sasa hadi tarehe 15 Machi, 2010. Pia tunapendekeza kuwa uwasilishaji wa makala uwe kwa Kiswahili, Kiingereza au Kijerumani. Kila uwasilishaji wa waraka utapewa dakika 30, zikiwemo dakika 10 za majadiliano. Wale ambao wanataka kushiriki katika kongamano bila

ya kuwasilisha warka, pia wanakaribishwa. Kongamano, kama kawaida, litafanyika *Iwalewa-Haus*, kituo cha Taaluma za Kiafrika katika Chuokikuu cha Bayreuth.

Kongamano hasa litaanza Ijumaa tarehe 14 Mei, 2010, saa 3 asubuhi na kumalizika Jumapili tarehe 16 Mei, 2010. Wakati hasa wa kumalizika utategemea idadi ya mchango wa makala tutakazozipokea na kuzikubali.

Wanafunzi watakaohudhuria kongamano watatakiwa kulipa ada ya usajili ya € 3, na wasiokuwa wanafunzi watatakiwa kulipa € 6.

Kama kawaida, siku ya mwanzo ya tarehe 13 Mei, 2010 ni siku ya kukutana mkahawani ili kabla ya kongamano kuanza tujane na wenzetu wapya, na pia tujue nani kafika na nani hajafika.

Suala la mkahawa gani, litaarifiwa katika barua yetu ya pili ya mwaliko baada ya kuchagua mkahawa mwafaka. Kama kawaida, wale watakaokula na kunywa chochote watalazimika kulipa wao wenyewe. Kwenye tovuti yetu:

http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/swahili_hotel/index.html, utakuta orodha ya hoteli na gesti ambazo utachagua kueleza nafasi. Gesti inayoitwa “Gasthaus zum Edlen Hirschen/Pension Elfert” – Richard-Wagner-Str. 77, D-95444 Bayreuth, nambari ya simu (+49-(0)921/764430), nambari ya Fax (+49(0)921/7644328), hutoa upungufu wa 10% kwa kila mgeni wa Chuokikuu cha Bayreuth.

Baadhi ya wanafunzi wetu hwenda wakawa tayari kutoa msaada kwa wanafunzi wenzao watakaokuja kushiriki katika kongamano. Wale ambao wanataka kupokea msaada huu watuletee mapema maombi ya kupata makaazi hayo.

Zaidi ya hayo, wale walio chini ya umri wa miaka 25, wanaweza kukaa kwa bei nafuu kwenye mabweni ya ‘Bayreuth Youth Hostel’. Kwa kupata habari zaidi kuhusu mabwenu hayo, tazama tovuti ifuatayo: <<http://www.jugendherberge.de/jh/bayern/bayreuth/>, Universitätstr. 28, nambari ya simu +49(0)921/764380.

Mwishoni mwa Aprili, tutatoa barua ya pili ya mwaliko itayoambatanishwa na ratiba ya mshikizo ya kongamano.

Ikiwa una masuala, tafadhali usisite kutuuliza. Tunapatikana kwenye baruapepe ifuatayo: Swahili@uni-bayreuth.de.

Tunasubiri kwa hamu kubwa kukukaribisha Bayreuth na pia katika Kongamano la Kiswahili la mwaka huu.

Ahsante,



Prof. Said A.M. Khamis
African Language Literatures
Universität Bayreuth
D-95440 Bayreuth
Tel: +49(0)921/55 3598
Fax: +44(0)921/553641



Prof. Gabriele Sommer,
Sprachen Afrikanistik I
Universität Bayreuth
D-95440 Bayreuth
Tel: +49(0)921/55 3656
Fax: +49(0)921/55 3627



Clarissa Vierke